# Ulega aagiza mifumo ya wafugaji kunenepesha ng'ombe ianzishwe

Na SCOLASTICA MSEWA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameiagiza Bodi ya Nyama Tanzania, kuanzisha mfumo mzuri utakaowasaidia wafugaji kunenepesha mifugo yao, ili wanufaike zaidi na fursa za masoko ya ndani na nje ya nchi kwakuwa mahitaji ya nyama ni makubwa.

Hayo aliyasema jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa mkutano maalumu na wafugaji wa kienyeji na wa kisasa na taasisi wezeshi za wafugaji, ambapo alisisitiza wafugaji wafuge kibiashara ili kutosheleza soko la ndani na nje.

Ulega alisisitiza kwamba elimu ya kutosha inapaswa iendelee kutolewa ili kuwajengea uwezo wafugaji wa kunenepesha mifugo yao, hata wale wanaofuga kienyeji ng'ombe, mbuzi na kondoo, kwa kuwa taifa limepata fursa kubwa za kibiashara katika nchi za Uarabuni, hivyo mahitaji ya nyama ni makubwa.

Aliagiza wafugaji wa halmashauri zote nchini wafundishwe namna moja ya kunenepesha na kuzalisha kwa wingi mifugo yao, huku wakijua soko la ndani na la nje linachotaka ni upatikanaji wa nyama bora na yenye thamani ya kimataifa itakayompa mfugaji faida kubwa.

Pia, alitaka bodi hiyo kutafuta namna ya kuwafundisha wafugaji wa asili wabadilike kwa kufuga kisasa zaidi, jambo litakalosaidia kuachana na ufugaji wa kuzurulisha mifugo, badala yake wafuge kwa ubora na katika mashamba ya ufugaji ili kukidhi viwango vya kimataifa.

Akizungumzia wafugaji kukopesheka katika benki, Ulega aliwasihi waingie mikataba na wenye viwanda vya kuchakata nyama kwa namna wanavyowasambazia mifugo yao ili wapate thamani ya kukubalika na kuaminiwa kupata fedha katika benki.

"Mikataba watakayopata itakuwa sehemu ya wao kukubalika wafugaji wapate fedha katika benki kwa lengo la kunenepesha mifugo yao ili waiuze katika soko la kimataifa na wapate fedha kwakuwa biashara ni nzuri sana," alisisitiza.

"Ukiandaa vizuri nyama yako mteja akiiona ni nzuri na yenye ubora, utafanya biashara maana soko lipo," alisema.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, hadi sasa viwanda vya kuchakata nyama za ng'ombe, mbuzi na kondoo nchini bado vinazalisha chini ya idadi iliyohitajika kutokana na kukosekana kwa idadi kubwa ya mifugo hiyo.

Naye, Ofisa Manunuzi wa kiwanda cha Tanchoice cha Kibaha, mkoani Pwani, Jabil Mohamed, alisema kiwanda chao kina uwezo wa kuchinja mbuzi 4,500 na ng'ombe 1000 kwa siku, hata hivyo wamekuwa wakipata mifugo kidogo ambapo wanachinja mbuzi hadi 2,000 na ng'ombe 150 kwa siku.

"Uzalishaji wetu ni wa kiwango kidogo sana ambacho ni sawa na asilimia 20 ya kiwanda chetu, hivyo wagufaji wanapaswa kuchangamkia fursa ya uwepo wa kiwanda hiki kwa kuwa kinaweza kuwatoa katika umasikini hadi kuwa matajiri," alisema Jabil na kubainisha kwamba kiwanda hicho mpaka sasa kina vibali vya kupeleka nyama katika nchi tano duniani.

Scanned with CamScanner

mpya ni jambo la umuhimu sana

Aidha, alisema ni vema Taifa likawa macho na baadhi ya watu

mpya ya kutaka kugawa CCM na kubadilisha kila siku kauli zao, wapinzani wamekuwa

chanjo hii inamadhara kama wanavyodai baadhi ya watu."

# Bil. 1.2/- kujenga soko la samaki la kimataifa Pangani

**Na Lulu George, TANGA**

*SERIKALI imetenga Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Samaki la Kimataifa katika Kijiji cha Kipumbwi, Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga.*

*Soko hilo litakuwa la pili hapa nchini likitanguliwa na lile la Feri lililopo Jiji la Dar es Salaam na mchakato wa ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwaka huu.*

*Hayo yalibainishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, wakati wa ziara ya kikazi kwenye Wilaya za Mkinga na Pangani mkoani Tanga.*

*Kwenye ziara hiyo alikagua majengo ya ofisi za vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (BMU) kwenye wilaya hizo yaliyojengwa chini ya Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).*

Waziri Ndaki alisema mradi wa soko hilo unatarajia kutumia kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi kwenye eneo la Mbegani,Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, kwamba unatarajiwa kuanza mapema mwaka huu.

Ndaki alisema kuwa serikali imekusudia kuhakikisha inaboresha sekta ya uvuvi ili iweze kuimarika na kuchangia katika pato la Taifa, kwa sasa imeanza mchakato wa ununuzi wa meli mbili za uvuvi kwa ajili ya kuvua samaki wakubwa kwenye bahari kuu.

Alisema kuwa kwa sasa serikali kupitia wizara hiyo inaimarisha miundombinu ambayo itakuwa ni kivutio cha wawekezaji hasa katika kujenga viwanda vya uchakataji wa samaki nchini badala ya kutegemea biashara moja tu ya kusafirisha samaki nje ya nchi.

Kuhusu kilimo cha Mwani, alisema kuwa wizara hiyo kwa sasa ina mpango wa kuwabaini wakulima wazoefu wa zao hilo ili kupitia Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO)waweze kupewa stadi na mbinu mbalimbali katika kuliongezea thamani zao hilo na kuliwezesha kumudu ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, akizungumza kuhusu gharama zilizotumika kwenye mradi huo wa majengo ya Ofisi za BMU alisema kuwa kwa upande wa Ofisi ya BMU Kijiji cha Zingibari Wilaya ya Mkinga zaidi ya Sh. milioni 155.118 zimetumika.

Scanned with CamScanner

# Bil 50/- kujenga Bandari ya Uvuvi Bagamoyo

Na Amina Omari, Pangani

SERIKALI imetoa Sh bilioni 51.2 za kujenga bandari ya uvuvi na soko la kimataifa la dagaa wilayani Bagamoyo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema hayo juzi alipokuwa akikagua majengo ya vikundi vya ulinzi shirikishi vya rasilimali za uvuvi (BMU) katika wilaya za Mkinga na Pangani, mkoani Tanga.

Majengo hayo yamejengwa kupitia mradi wa Swiofish unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Ndaki alisema Sh bilioni 50 zimetolewa na serikali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mbegani, wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Alisema bandari hiyo itaboresha kipato cha wananchi na kutengeneza fursa za ajira kwani meli kubwa za uvuvi katika bahari kuu zitatia nanga katika bandari hiyo.

"Kwa sasa serikali inapata mapato ya kodi ya kibali cha uvuvi pekee kwa wavuvi wanaovua katika bahari kuu, lakini baada ya bandari hiyo kukamilika meli zitalazimika kutia nanga katika bandari yetu na kuchakata samaki hapa hapa nchini na wataondoka na bidhaa pekee, hivyo tutakuwa tumetoa fursa za ajira kwa wananchi wetu lakini na serikali imepata mapato yake," alisema Ndaki.

Aidha, alisema serikali itatoa Sh bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kimataifa la dagaa katika eneo la Kipumbwi, wilayani Pangani ili kuongeza masoko ya samaki nchini.



Ndaki alisema eneo la ukanda wa bahari nchini ni kubwa na soko la Kipumbwi litakuwa la pili la kimataifa kwenye eneo hilo.

Alisema usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi umesaidia kuboresha mazingira ya bahari na ndio maana serikali inawekeza katika sekta hiyo ili kukuza uchumi.

"Licha ya fursa za rasilimali za bahari zilizopo lakini bado hatujaweza kuzitumia vizuri, kwa uwekezaji unaoenda kufanywa na serikali tutaweza kupata kipato cha uhakika kwa wananchi wetu lakini na nchi kwa ujumla," alisema Ndaki.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah alisema mradi wa Swiofish umesaidia kujenga ofisi ya BMU katika wilaya tano nchini ili kuwezesha wavuvi washirikiane na serikali kwenye utunzaji wa rasilimali za bahari na kutumia zana bora za uvuvi kwa ajili ya kufanya shughuli za uvuvi zenye tija bila ya uharibifu.

Alisema mradi wa Swiofish unajenga ofisi za BMU katika wilaya za Mkinga – Zingibari, Pangani – Kipumbwi; Chalinze – Saadan, Bagamoyo – Dunda na Lindi Vijijini – Sudi.

Alisema pia mradi huo umejenga maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (Tafiri) Kunduchi, Dar es Salaam na ujenzi wa nyumba tatu za watumishi wa Hifadhi ya Silikanti, Kigombe, Tanga.

Scanned with CamScanner

# Minister tells meat board to create pastoralists database

**Lack of livestock despite boasting large numbers in Africa has left many investors in the meat area counting losses**

By Halili Letea
@hletea
hletea@tz.nationmedia.com

**Dar es Salaam.** The ministry for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega, has directed the Tanzania Meat Board (TMB) to have a specified database of livestock keepers so that it can be easy to link them with other value chain stakeholders.

Mr Ulega issued the statement on Monday evening during a meeting with livestock keepers, meat processors and other sectorial members.

"There is a big opportunity and a large market of meat from local processors and overseas, but we don't have a specified database which will enable customers to know where to get those products" he said, adding that the board is proud of having enough cattle.

A procurement officer from Soga–Kibaha based modern meat factory TanChoice Limited, Jabiri Mohamed, said they were operating below capacity due to lack of livestock.

"We have a capacity of processing 1,000 cattle and 4,000 goats and sheep per day, but we only process 2,500 goats and sheep and only up to 150 cattle a day," he said, adding that the main problem is lack of the availability of quality livestock from local keepers.



Livestock and Fisheries Deputy minister Abdallah Ulega (right) speaks to stakeholders of the livestock sector during a meeting in Dar es Salaam yesterday. PHOTO|ERICKY BONIPHACE

Another representative from Eliya Food Overseas Tanzania, a factory from Arusha Region, Mr Karim Kika, said they have

Scanned with CamScanner

a wahitimu wenye ujuzi
kukabiliana na kuyapa-
tumbuzi matatizo ya
ii na kiuchumi.
Mataka taasisi za elimu
zisiwe waathirika wa

ukanda wa EAC katika
kukabiliana na changamoto
za kijamii na kiuchumi.
"Ni vema IUCEA ku-
waunganisha wanasayansi

ni kuhakikisha mitaala ya
elimu ya vyuo vikuu katika
Jumuiya ya Afrika Mashari-
ki inaendana na soko la

wenye ustadi mkubwa
unaolingana na mahitaji ya
viwanda," alisema Profesa
Banyankimbona.

## ...a mkakati ...i duniani

...daji wa TSN, Tuma
...llah alimwelezea Waziri
mkakati wa kampuni
katika kukuza na ku-
...isha kimapato, pamoja
...uza lugha ya Kiswahili
...i fursa za vyombo vya
...vya nje.
...mejipanga kukuza
...a Kiswahili nje ya nchi
vyombo vya habari
...ataifa yaliyotayari
lugha hiyo kama seh-
...wapo ya kuongeza
na pia kuipanua
...dhimu, tumesha-
...i na baadhi yao na
...oyatari," alisema

...yo alisema pamoja
...a kukua, sekta
...i mawasiliano
...ngamoto mbalim-
...uchapaji wa
...okana na hivi
...eegemea zaidi
...i za kidijitali.
...nzia jinsi TSN
...a na changa-
...a alisema
...oresha kitengo
...i na uchapaji
...nbamba na
ili kuwavutia
...angazaji.
...isema
...a changa-
...atumizi ya
...a habari na
...a TSN ita-
...ri kwenye
...ijitali.
kuangalia
...na serikali
...noto ya
...tali na
...a TSN
...zuri katika
...ijitali kwa
...muhimu
...anchi
...hungwa.

# Tanzania kushughulikia ushuru wa maziwa unaolalamikiwa EAC

**Na Theopista Nsanzugwanko**

TANZANIA imezihakikishia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa inafanyia kazi ushuru wa maziwa unaoalalamikiwa kuwa kikwazo kwa nchi hizo kufanya biashara ya bidhaa hiyo nchini.

Imeelezwa kuwa, baada ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Kenya na kutoa maelekezo ya kuondolewa vikwazo vya biashara, kulifanyika kikao mkoani Arusha kwa lengo la kuondoa vikwazo vya biashara na ushuru wa maziwa uliokuwa na changamoto katika ufanyaji biashara.

Mwanasheria wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Edwin Bantulaki alisema juzi kuwa, baada ya kuelezwa changamoto hizo, Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na bodi hiyo walifanya tathmini ya ushuru huo unaotozwa kwa nchi zote zinazoingiza maziwa nchini na kuangalia athari na faida za tozo hiyo.




Alisema hatua hiyo ilichukuliwa baada ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Uganda kupitia barua yake ya Julai 19, mwaka huu iliyoandikwa na Waziri wa wizara hiyo, Frank Tumwebaze kuzilalamikia Tanzania na Kenya kuwa na vikwazo vya kuingiza bidhaa za maziwa kutoka nchi hiyo.

Alisema tangu mwaka jana, Uganda ilifanya jitihada kuuza bidhaa za maziwa katika nchi hizo lakini ilipata wakati mgumu kutokana na vikwazo katika ushuru licha ya kufanya majadiliano na viongozi wa nchi hizo bila mafanikio.

Katika barua yake kwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Tanzania, Profesa Adolf Mkenda, alisema Tanzania hutoza Sh 2,000 ambazo ni changamoto kwa nchi hiyo kuuza maziwa nchini.

Tumwebaze alilalamikia asilimia 1.75 ya ushuru na Sh 30, 000 (takribani Sh 46,000 za Uganda) kama tozo ya maombi katika Bodi ya Maziwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa bidhaa zote za maziwa.

"Licha ya ukweli kuwa majadiliano mengi yamefanyika kati ya Uganda na Tanzania na kupewa ahadi ya kuondoa lakini haikutekelezwa ikiwamo ada ya Sh 2,000 inayotozwa na wizara," alisema Tumwebaze.

Akielezea



Mwanasheria wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Edwin Bantulaki.

hatua zilizochukuliwa katika suala hilo la kodi za maziwa, Bantulaki alisema tayari wamepeleka mapendekezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo ili kuangalia suala hilo na kuzitaka nchi za Kenya na Uganda kuwa na subira.

Alisema changamoto hiyo ilielezwa hata kwa wafanyabiashara wa Kenya na kuanza kufanyiwa kazi kwa kuanzia katika kikao kilichofanyika Arusha na kuafikiana katika kupunguza tozo hiyo lakini wakakubaliana kubadili sheria katika miezi mitatu.

"Malalamiko haya yameishafikia wizara na yanaendelea kufanyiwa kazi hivyo ni vema Kenya na Uganda na nchi nyingine kuwa na subira wakati serikali inafanyia kazi na itakuja na majibu mazuri katika kuwezesha kufanya biashara," alisema.

Scanned with CamScanner